# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

## FOMATI ZA MITIHANI YA UALIMU KWA NGAZI YA CHETI
## (DARAJA LA A)

**IMETOLEWA NA:**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**S.L.P. 2624**
**DAR ES SALAAM**
**TANZANIA**

**SEPTEMBA 2010**

## YALIYOMO

UTANGULIZI .......... ii
610 UALIMU .......... 1
612 URAIA .......... 3
614 MAARIFA YA JAMII .......... 5
616 MBINU ZA KUFUNDISHIA ELIMU YA DINI YA KIISLAMU .......... 7
621 KISWAHILI .......... 9
622 ENGLISH LANGUAGE .......... 11
623 FRENCH LANGUAGE .......... 13
624 COMMUNICATION SKILLS .......... 15
632 SAYANSI .......... 16
634 STADI ZA KAZI .......... 18
636 TEHAMA .......... 20
638 VIELELEZO NA TEKNOLOJIA .......... 22
640 HISABATI .......... 24
650 HAIBA NA MICHEZO .......... 26

## UTANGULIZI


Fomati hizi mpya za Mitihani ya Ualimu kwa Ngazi ya Cheti (Daraja la A) imeandaliwa kwa kuzingatia marekebisho ya mtaala wa Ualimu Ngazi ya Cheti yaliyofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi mwaka 2009. Mabadiliko katika mtaala mpya ni pamoja na kuunganisha masomo ya Saikolojia ya Elimu na Kunasihi, Utafiti wa Kielimu, Upimaji na Tathimini, Misingi ya Elimu na Mitaala na Ufundishaji kuwa somo moja la Ualimu. Pia mada za Taaluma zimeingizwa katika mtaala mpya sambamba na mada za kufundishia masomo husika. Aidha, somo la Mbinu za Kufundishia Maarifa ya Jamii limetenganishwa na kuwa na masomo ya Historia na Jiografia yanayojitegemea. Hata hivyo, masomo hayo yatatahiniwa kwa mtihani mmoja wa Maarifa ya Jamii ambao utakuwa na maswali yenye uwiano sawa ya Historia na Jiografia.

Badiliko jingine katika mtaala mpya ni kuanzishwa kwa masomo ya Uraia, Kiswahili, English Language, TEHAMA, Haiba na Michezo, Hisabati, Sayansi na Stadi za Kazi. Aidha wanachuo wanaruhusiwa kuchagua somo mojawapo kati ya Vielelezo na Teknolojia, Communication Skills na French Language ambayo pia ni masomo mapya. Lengo kuu la mabadiliko katika mtaala ni kumjengea mwanachuo uwezo wa kufundisha kinadharia na kivitendo masomo yote yanayofundishwa katika shule za msingi pamoja na kuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali toka kwa wanafunzi.

Fomati hii imeandaliwa kwa kuzingatia mada zilizomo katika mihtasari mipya ya masomo yanayofundishwa katika Vyuo vya Ualimu Ngazi ya Cheti (Daraja la A) ili kutoa mwongozo kwa Wanachuo na Wakufunzi kuhusu muundo wa mtihani. Wakufunzi na Wanachuo wanashauriwa kutotumia fomati hii kama mbadala wa mihtasari. Katika ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mada zote zilizoainishwa katika mihtasari ya Mafunzo ya Ualimu zifundishwe kikamilifu.

Fomati ya kila somo inaonesha Utangulizi, Ujuzi wa jumla na Ujuzi Mahususi utakaopimwa, Muundo wa Mtihani na Maudhui ya Mtihani. Aidha muda wa kufanya mtihani kwa kila somo umeoneshwa. Watahiniwa wasioona na wale wenye uoni hafifu wataongezewa muda wa ziada wa kufanya mtihani wa dakika 10 kwa kila saa kwa masomo yote ya Sanaa, Lugha, Sayansi na TEHAMA na dakika 20 kwa kila saa kwa somo la Hisabati.

Fomati hizi mpya zitaanza kutumika katika mitihani ya Mei 2011. Baraza la Mitihani linatoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani wote walioshiriki katika kuandaa fomati hii. Aidha, Baraza la Mitihani litakuwa tayari kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa watumiaji wa fomati hizi yenye lengo la kuziboresha zaidi.



Dkt. Joyce L. Ndalichako
**KATIBU MTENDAJI**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# 610 UALIMU

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya mtihani wa somo la Ualimu imeandaliwa ili kwenda sanjari na mada zilizomo katika muhtasari mpya wa Ualimu Ngazi ya Cheti wa mwaka 2009. Mtihani wa ualimu unaweka mkazo katika kupima ujuzi, stadi na mbinu zinazotakiwa ili kumudu mada mbalimbali zinazofundishwa katika masomo yote kwa ngazi ya shule za msingi. Somo la Ualimu linatokana na kuunganishwa kwa masomo ya Saikolojia ya Elimu, Upimaji na Tathmini, Misingi ya Elimu na Mitaala na Ufundishaji.

## 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa somo la Ualimu unalenga kupima ujuzi wa watahiniwa katika:

2.1 kuelewa dhana, nadharia, kanuni na stadi mbalimbali alizojifunza katika somo la ualimu.

2.2 kutambua maarifa na stadi za utafiti katika kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji.

2.3 kuelewa maarifa na stadi zinazohitajika katika uongozi wa elimu na uendeshaji wa shule.

2.4 kukuza uelewa na stadi zinazohusu elimu jumuishi na elimu ya watu wazima.

## 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani wa somo la Ualimu unalenga kupima ujuzi wa watahiniwa katika:

3.1 kutumia nadharia na kanuni mbalimbali za kujifunza katika ufundishaji na ujifunzaji.

3.2 kutumia mbinu na stadi za kunasihi katika kurekebisha mienendo na tabia za wanafunzi ili waweze kujifunza kwa ufanisi.

3.3 kutumia stadi za upimaji na tathmini katika elimu ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

3.4 kutumia ujuzi na mitaala katika kuyatayarisha masomo na kuyafundisha kwa kuzingatia watoto wenye mahitaji maalum ili kuwasaidia wajifunze zaidi.

3.5 kuchambua mwelekeo na falsafa na maendeleo ya elimu nchini Tanzania kwa kuzingatia mahitaji ya Taifa.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa somo la Ualimu utakuwa na sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **kumi na nane (18).** Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne (14).** Muda wa mtihani utakuwa ni saa **tatu (3)**. Sehemu A itakuwa na maswali **kumi** (**10**) yenye jumla ya alama **arobaini** (**40**) na mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali yote. Maswali yatakuwa ya majibu mafupi na yatakayotungwa kutoka kwenye mada yoyote ya somo la Ualimu. Sehemu B, C, D na E zitakuwa na maswali mawili ya insha kwa kila moja. Sehemu zinatokana na maeneo makuu ya Saikolojia ya Elimu, Upimaji na Tathmini, Misingi ya Elimu na Mitaala na Ufundishaji. Mtahiniwa atatakiwa kujibu swali moja katika kila sehemu na jumla ya alama kwa swali zitakuwa ni **kumi na tano** (**15**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani, mada kuu zifuatazo zitazingatiwa:

### 5.1 MADA ZA SAIKOLOJIA YA ELIMU

5.1.1 Saikolojia
5.1.2 Makuzi na Ukuaji wa Mtoto
5.1.3 Nadharia za Kujifunza
5.1.4 Ushauri na Unasihi

### 5.2 MADA ZA MITAALA NA UFUNDISHAJI

5.2.1 Mtaala
5.2.2 Matayarisho ya Ufundishaji
5.2.3 Ufundishaji

### 5.3 MADA ZA UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI

5.3.1 Upimaji katika Elimu
5.3.2 Tathmini katika Elimu
5.3.3 Utafiti wa Kielimu

### 5.4 MADA ZA MISINGI YA ELIMU

5.4.1 Taaluma ya Ualimu
5.4.2 Maendeleo ya Elimu Tanzania
5.4.3 Uongozi wa Elimu Tanzania
5.4.4 Elimu Jumuishi
5.4.5 Elimu ya Watu Wazima

## 612 URAIA

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati ya mtihani wa somo la Uraia imeandaliwa kwa mara ya kwanza kutokana na maboresho yaliyofanywa katika muhtasari wa somo la Uraia kwa Vyuo vya Ualimu nchini mwaka 2009. Katika maboresho hayo, mada za mbinu za kufundishia somo la Uraia zimeingizwa kwenye mtaala ili kuwajengea uwezo wahitimu katika kumudu ufundishaji wa somo hilo. Hivyo, Fomati hii inalenga katika kutoa mwongozo wa namna ya kupima uwezo wa wahitimu kutumia ujuzi, stadi na mbinu shirikishi katika hatua mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia.

## 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa somo la Uraia utalenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika:

2.1 kumudu maudhui ya mada za somo la Uraia na masuala mtambuka.
2.2 kufundisha kwa kuzingatia umuhimu wa kuwajengea wanafunzi uzalendo, haiba na uwezo wa kutumia teknolojia katika kujitafutia maarifa.
2.3 kuchambua vifaa vya mtaala wa somo la Uraia.
2.4 kuunda zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia.
2.5 kuandaa maazimio ya kazi, maandalio ya somo, nukuu za somo za kufundishia na kujifunzia.
2.6 kutumia elimu ya uraia katika kuongeza stadi za juu za kufikiri.

## 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani wa somo la Uraia utapima ujuzi wa mtahiniwa wa:

3.1 kuandaa vipindi kwa kutumia mbinu shirikishi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia.
3.2 kutengeneza na kufaragua zana na vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia.
3.3 kuchambua na kutumia zana/vifaa muhimu vya mtaala wa Uraia.
3.4 kumudu maudhui / mada za kitaaluma zilizoainishwa katika muhtasari wa somo la Uraia kwa shule za Msingi.
3.5 kufanya upimaji na tathmini ya wanafunzi na kuweka kumbukumbu za matokeo ya kazi za wanafunzi na kutoa taarifa kwa wadau.
3.6 kukuza maendeleo ya kihaiba, kizalendo, kiteknolojia na ubunifu katika ufundishaji wa somo la Uraia.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa somo la Uraia utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na nane (18)**. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne (14).** Muda wa mtihani utakuwa ni saa **tatu (3)**.

4.1 **Sehemu A** itakuwa na jumla ya maswali **kumi (10)** ya majibu mafupi ambayo yanajumuisha maswali ya taaluma na njia za kufundisha na kujifunzia somo la Uraia. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote** na jumla ya alama zitakuwa ni **arobaini** (**40**).

4.2 **Sehemu B** na **C** zitakuwa na maswali matatu ya insha kwa kila sehemu, ambapo mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu. Maswali ya sehemu B yatatahini mada za taaluma

ya somo la Uraia na sehemu C itatahini mbinu za kufundishia somo la Uraia. Jumla ya alama katika kila sehemu zitakuwa ni **thelathini (30).**

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani, mada zifuatazo zitazingatiwa:

### 5.1 TAALUMA YA URAIA

5.1.1 Dola
5.1.2 Utamaduni wetu
5.1.3 Uchumi wa Tanzania
5.1.4 Uhusiano wa kimataifa

### 5.2 UFUNDISHAJI WA SOMO LA URAIA

5.2.1 Misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la uraia.
5.2.2 Uchambuzi wa maandiko/machapisho muhimu ya kufundishia/kujifunzia somo la uraia.
5.2.3 Zana za kufundishia na kujifunzia.
5.2.4 Maandalizi ya kufundisha somo la uraia.
5.2.5 Upimaji na tathmini katika somo la uraia.

## 614 MAARIFA YA JAMII

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati ya mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii imeandaliwa kutokana na maboresho ya mwaka 2009 yaliyofanywa katika mihtasari ya somo la Historia na somo la Jiografia kwa Vyuo vya Ualimu nchini ambapo mada za taaluma za somo husika zimeongezwa. Kabla ya mwaka 2009 masomo haya yalitahiniwa katika karatasi ya Mbinu za Kufundishia Maarifa ya Jamii ambayo ilijikita katika kupima uwezo wa wahitimu wa Mafunzo ya Ualimu katika matumizi ya mbinu na njia anuwai za kufundishia. Katika utahini, mtihani utakuwa ni mmoja unaojumuisha mada za somo la Historia na Jiografia kwa uwiano sawa.

## 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii utapima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 kuelewa stadi na ujuzi wa mbinu shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Historia na Jiografia.

2.2 kujifunza mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji zinazozingatia usawa wa kijinsia, kinadharia na vitendo katika masomo ya Historia na Jiografia.

2.3 kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuwa na mwelekeo chanya kuhusu masomo ya Historia na Jiografia.

2.4 kuelewa stadi, ujuzi na maarifa katika kutoa ushauri nasaha, elimu maalumu na masuala mtambuka.

2.5 kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu katika masomo ya Historia na Jiografia.

2.6 kufahamu stadi na mbinu za utafiti katika mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

## 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii utapima uwezo wa mtahiniwa wa:

3.1 kutumia stadi na ujuzi katika kufundisha na kutoa ushauri katika masuala mtambuka.

3.2 kuandaa masomo kwa kutumia mbinu shirikishi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Historia na Jiografia.

3.3 kutengeneza na kufaragua zana na vifaa mbalimbali vya kufundishia/kujifunzia masomo ya Historia na Jiografia.

3.4 kuwaongoza wanafunzi katika kukusanya na kutengeneza zana na vifaa vya kujifunzia.

3.5 kumudu maudhui/mada za kitaaluma zilizoainishwa katika muhtasari wa somo la Historia na Jiografia.

3.6 kuchambua na kutumia zana na vifaa katika kufundishia mada zilizoainishwa katika muhtasari wa Historia na Jiografia katika shule za Msingi.

3.7 kufanya upimaji wa wanafunzi na kuweka kumbukumbu za matokeo ya kazi za wanafunzi na kutoa taarifa kwa wadau.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

4.1 Mtihani wa Maarifa ya Jamii utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na nane** (**18**). Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne** (**14**). Muda wa mtihani utakuwa ni saa **tatu** (**3**).

4.2 **Sehemu A** itakuwa na maswali **kumi** (**10**) yenye jumla ya alama **arobaini** (**40**). Maswali **matano** (**5**) yatatoka katika somo la Historia na **matano** (**5**) katika somo la Jiografia, mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote** katika sehemu hii.

4.3 **Sehemu B** itakuwa na maswali **manne** (**4**) ya insha yatakayotahini mada za taaluma ya somo la Historia na Jiografia kwa uwiano ulio sawa. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **mawili** (**2**), yenye jumla ya alama **thelathini** (3**0**).

4.4 **Sehemu C** itakuwa na maswali **manne** (**4**) ya insha kutoka katika mada za kufundishia masomo ya Historia na Jiografia kwa uwiano ulio sawa. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **mawili** (**2**), moja likiwa linahusu somo la Historia na lingine la Jiografia. Jumla ya alama katika sehemu hii ni **thelathini** (3**0**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

### 5.1 TAALUMA YA HISTORIA NA JIOGRAFIA

Katika kuandaa mtihani zitazingatiwa mada zifuatazo:

5.1.1 asili na mabadiliko ya binadamu, teknolojia na mazingira
5.1.2 vitangulizi vya ukoloni Tanganyika, Zanzibar na kwingineko Afrika
5.1.3 upinzani dhidi ya uvamizi wa kikoloni Afrika
5.1.4 utawala na uchumi wa kikoloni Afrika
5.1.5 ukombozi wa bara la Afrika
5.1.6 mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi katika Afrika huru
5.1.7 ushirikiano wa kimataifa
5.1.8 sayari dunia
5.1.9 nchi yetu Tanzania
5.1.10 stadi sahili na tata za picha na ramani

### 5.2 UFUNDISHAJI WA SOMO LA HISTORIA NA JIOGRAFIA

Katika kuandaa mtihani mada zifuatazo zitazingatiwa:

5.2.1 misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Historia na Jiografia.
5.2.2 uchambuzi wa vifaa na zana za kufundishia/kujifunzia somo la Historia na Jiografia.
5.2.3 kujiandaa kwa ajili ya kufundisha somo la Historia na somo la Jiografia.
5.2.4 ufundishaji wa mada za somo la Historia na somo la Jiografia.
5.2.5 upimaji na tathmini katika somo la Historia na somo la Jiografia.

## 616 MBINU ZA KUFUNDISHIA ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

### 1.0 UTANGULIZI

Marekebisho yaliyofanywa katika Fomati ya Mtihani wa Mbinu za Kufundishia Elimu ya Dini ya Kiislamu katika ngazi ya Cheti yamelenga katika kuwa na karatasi moja ya mtihani badala ya karatasi tatu za awali. Karatasi hiyo ya mtihani itazingatia uwepo wa maudhui makuu matatu yaliyokuwa yakitahiniwa kwenye karatasi tatu za awali ambayo ni Tawhiid, Fiqh na Tarekh.

### 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa Mbinu za Kufundishia Elimu ya Dini ya Kiislamu utapima ujuzi wa mtahiniwa katika:

2.1 kufafanua lengo la maisha ya mwanadamu na hadhi yake.
2.2 kutambua mitizamo juu ya Uislamu na mifumo ya maisha ya jamii ya Kiislamu.
2.3 kuelezea mafunzo ya Qur'an.
2.4 kuwa na ujuzi juu ya mambo yahusuyo Tawhiid, Fiqh na Tarekh ili kuendeleza na kudumisha Uislamu.
2.5 kufundisha Elimu ya Dini ya Kiislamu.
2.6 kupima na kutathmini kazi za wanafunzi.

### 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani utapima uwezo wa watahiniwa katika:

3.1 kueleza mtizamo wa Uislamu juu ya Elimu na Dini ya Kiislamu.
3.2 kueleza lengo la maisha ya mwanadamu, hadhi na dhima katika jamii kwa mujibu wa Qur'an.
3.3 kuchambua nguzo tano za Uislamu na nguzo sita za imani ya Kiislamu.
3.4 kuchambua Qur'an kama kitabu chenye mafunzo mema.
3.5 kuchambua na kubaini mafunzo yatokanayo na Sunnah na Hadith.
3.6 kuainisha mfumo wa maisha ya familia na jamii ya Kiislamu.
3.7 kutathmini historia na mafunzo yatokanayo na historia ya Mitume waliotajwa katika Qur'an.
3.8 kueleza maana na umuhimu wa Da'awah na kuainisha mbinu za kulingania uislamu kwa ufanisi.
3.9 kubainisha malengo na namna ya kufundisha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu pamoja na kutumia mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji wa Qur'an.
3.10 kuchambua vifaa vya mtaala vya somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.
3.11 kupima na kutathmini kazi za wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

### 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa Mbinu za Kufundishia Elimu ya Dini ya Kiislamu utakuwa na karatasi **moja (1)** itakayokuwa na maudhui makuu ya Tawhiid, Fiqh na Tarekh. Karatasi ya mtihani itakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **ishirini (20).** Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne (14)** kwa muda wa saa **tatu (3)**.

4.1 **Sehemu A** itakuwa na maswali **nane (8)** yenye jumla ya alama **arobaini** (**40**) yatakayotahini Fiqh, Tawhiid na Tarekh. Mtahiniwa atajibu maswali yote.

4.2 **Sehemu B** itakuwa na maswali **sita (6)** ya insha kutoka mada za Fiqh, Tawhiid na Tarekh. Mtahiniwa atajibu swali moja kutoka katika kila maswali mawili ya mada hizo. Mtahiniwa atajibu jumla ya maswali **matatu (3)** yenye alama **thelathini** (**30**).

4.3 **Sehemu C** itakuwa na maswali **sita (6)** ya insha kutoka mada za Fiqh, Tawhiid na Tarekh. Mtahiniwa atajibu swali moja kutoka katika kila maswali mawili ya mada hizo. Mtahiniwa atajibu jumla ya maswali **matatu (3)** yenye alama **thelathini** (**30**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani mada zifuatazo zitazingatiwa:

### 5.1 Tawhiid

5.1.1 Mtizamo wa uislamu juu ya elimu
5.1.2 Lengo la maisha ya mwanadamu na hadhi yake hapa duniani
5.1.3 Imani ya Kiislamu
5.1.4 Qurȃan
5.1.5 Sunnah na hadith
5.1.6 Ufundishaji wa elimu ya dini ya kiislamu katika shule za msingi
5.1.7 Vifaa vya mtaala vya somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu

### 5.2 Fiqh

5.2.1 Nguzo za uislamu
5.2.2 Mfumo wa maisha ya familia ya Kiislamu
5.2.3 Mfumo wa maisha ya jamii ya Kiislamu
5.2.4 Maandalizi ya kufundisha somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu
5.2.5 Zana za kufundishia somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu

### 5.3 Tarekh

5.3.1 Historia ya mitume wa Allah (s.w) kabla ya Mtume (s.a.w)
5.3.2 Historia ya uislamu wakati wa Mtume (s.a.w)
5.3.3 Historia ya uislamu baada ya Mtume hadi hivi leo
5.3.4 Daȃawah
5.3.5 Tathmini na upimaji

## 621 KISWAHILI

## 1.0 UTANGULIZI

Fomati ya mtihani wa Kiswahili ngazi ya Cheti imeandaliwa kutokana na maboresho yaliyofanywa katika muhtasari wa somo la Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu nchini mwaka 2009. Fomati hii itatoa mwongozo wa namna ya kupima uwezo wa wahitimu kutumia ujuzi, stadi na mbinu shirikishi katika hatua mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili.

## 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa Kiswahili unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 kukuza uelewa wa mbinu anuai zinazomshirikisha mwalimu na mwanafunzi katika kufundisha na kujifunza somo la Kiswahili.
2.2 kuelewa vipengele mbalimbali vya taaluma ya somo la Kiswahili.
2.3 kuchambua muhtasari na vifaa vya muhtasari wa somo la Kiswahili.
2.4 kupima na kutathmini maendeleo ya ujifunzaji wa Kiswahili na kutoa mrejesho.

## 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani utakaotungwa utalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

3.1 kuchambua mada mbalimbali za somo la Kiswahili, zinazofundishwa katika shule za msingi.
3.2 kutumia msamiati na miundo ya Kiswahili kwa usahihi katika maandishi.
3.3 kutumia njia shirikishi katika ufundishaji wa somo la Kiswahili.
3.4 kutumia, kuchambua, kuunda na kutathmini stadi mbalimbali zilizomo kwenye muhtasari wa Kiswahili.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa Kiswahili utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na nane** (**18**). Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne** (**14**) Muda wa mtihani ni saa **tatu** (**3**).

4.1 **Sehemu A** itakuwa na maswali **kumi** (**10**) kutoka kwenye taaluma na njia za ufundishaji. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Jumla ya alama itakuwa ni **arobaini (40)**.

4.2 **Sehemu B** itakuwa na maswali **manne (4)** ya insha kutoka kwenye maudhui ya taaluma ya somo la Kiswahili. Mtahiniwa atajibu maswali **mawili** (**2**). Jumla ya alama ni **thelathini** (**30**).

4.3 **Sehemu C** itakuwa na maswali **manne** (**4**) ya insha kutoka kwenye mada za njia za ufundishaji wa somo la Kiswahili. Mtahiniwa atajibu maswali **mawili (2).** Jumla ya alama ni **thelathini** (**30**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani mada zifuatazo zitazingatiwa:

5.1 Stadi za lugha
5.2 Utungaji
5.3 Fasihi simulizi
5.4 Ufahamu
5.5 Sarufi
5.6 Mbinu za kufundishia na kujifunzia Kiswahili
5.7 Uchambuzi wa vifaa vya mtaala wa Kiswahili
5.8 Maandalizi ya kufundisha somo la Kiswahili
5.9 Zana za kufundishia na kujifunzia Kiswahili
5.10 Upimaji
5.11 Ufundishaji wa mada teule za somo la Kiswahili

## 622 ENGLISH LANGUAGE

## 1.0 INTRODUCTION

The English Language Examination Format has been revised to accommodate the changes made in the 2009 English Language Syllabus for the Grade A Certificate Course. The main changes include the shift from emphasis on content to competence-based instruction and the inclusion of academic content in concurrent pedagogy.

## 2.0 GENERAL COMPETENCES

The English Language examination will measure candidateŏs ability to:

2.1 use English Language effectively in various situations/settings.
2.2 develop and apply the four language skills: Listening, Speaking, Reading and Writing.
2.3 demonstrate mastery of forms, functions and meanings of the English Language.
2.4 upgrade academic knowledge to cope up with on going changes and advancements.

## 3.0 SPECIFIC COMPETENCES

The examination will test the candidatesô ability to:

3.1 apply the four language skills: Listening, Speaking, Reading and Writing.
3.2 use English Language effectively in various situations/settings.
3.3 upgrade academic knowledge to cope up with ongoing changes and advancements.
3.4 construct new Teaching/Learning materials.
3.5 apply suitable methods and strategies, as learnt in their course, in teaching and learning process.
3.6 utilize scientific skills and technology in everyday life.
3.7 apply participatory approaches in the teaching and learning of English Language.

## 4.0 EXAMINATION RUBRIC

English Language examination will consist of **eighteen (18)** questions in sections A, B and C. The candidates will be required to answer **fourteen (14)** questions. The duration of the paper will be **three (3)** hours.

4.1 **Section A** will consist of **ten (10)** short answer questions from both academic and pedagogy topics. The candidates will be required to answer **all** the questions in this section. The section will carry **forty (40)** marks.

4.2 **Section B** will consist of **four** (**4**) essay type questions from the academic part. The candidates will be required to answer **two (2)** questions which will carry **thirty** (**30**) marks.

4.3 **Section C** will consist of **four** (**4**) essay type questions from pedagogy. The Candidates will be required to answer **two** (**2**) questions which will carry **thirty** (**30**) marks.

## 5.0 EXAMINATION CONTENT

In setting the examination, the following topics will be considered:

5.1 Expressing habits/ frequency
5.2 Expressing past events
5.3 Reporting events
5.4 Expressing contrasts
5.5 Expressing possessions
5.6 Expressing likelihood and certainity
5.7 Expressing conditions
5.8 Expressing time of action
5.9 Expressing purpose and results
5.10 Reading literary works
5.11 The role of English Language
5.12 Principles of English Language teaching and learning
5.13 Teaching pronunciation, vocabulary and structural pattern
5.14 Developing English Language skills
5.15 Analyzing the primary school English Language syllabus
5.16 Preparing for teaching and assessment

## 623 FRENCH LANGUAGE

### 1.0 INTRODUCTION

This examination format is based on the French syllabus: PROGRAMME DU CERTIFICAT DE LøÉDUCATION POUR LøENSEIGNMENT DANS LES ÉCOLES PRIMAIRES. The syllabus issued in 2009 aims at developing the traineesô linguistic and pedagogical competences. Therefore the French Language Format has been revised to accommodate, accordingly, the changes made in the syllabus.

### 2.0 GENERAL COMPETENCES

The French Language examination shall test candidates:

2.1 linguistic competences.
2.2 ability to prepare and conduct lessons.
2.3 ability to use different teaching methods and evaluate them.
2.4 ability to evaluate both studentsô understanding and the effectiveness in teaching.
2.5 knowledge of African literature in French language.

### 3.0 SPECIFIC COMPETENCES

The examination will measure the candidateøs ability to:

3.1 pronounce the French sounds properly.
3.2 communicate effectively in French language.
3.3 express themselves fluently in French language.
3.4 use and evaluate different teaching methods.
3.5 analyse the syllabus and other curriculum materials.
3.6 prepare teaching documents such as lesson plan and scheme of work.
3.7 prepare and to use teaching materials appropriately.
3.8 prepare and to conduct lesson.

### 4.0 EXAMINATION RUBRIC

The French Language examination will consist of **eighteen** (**18**) questions in sections A, B and C. The candidates will be required to answer **fourteen** (**14**) questions. The duration of the examination will be **three (3)** hours.

**Section A** will consist of **ten (10)** short answer questions from both academic and pedagogy topics. Candidates will be required to answer **all** the question. The total marks will be **forty (40)**.

4.1 **Section B** will consist of **four (4)** essay questions from the academic part. Candidates will be required to answer **two (2)** questions which will carry **thirty (30)** marks.

4.2 **Section C** will consist of **four (4)** essay questions from pedagogy. The Candidates will be required to answer **two (2)** questions which will carry **thirty (30)** marks.

## 5.0 EXAMINATION CONTENT

In setting the examination, the following topics will be considered:

### 5.1 French Language Content

5.1.1 Prononciation
5.1.2 Lôalphabet
5.1.3 Utilisation des dictionnaires
5.1.4 Compréhension orale et écrite
5.1.5 Expression orale et écrite
5.1.6 Usage de langue
5.1.7 Etude de textes littéraires

### 5.2 French Language Pedagogy

5.2.1 La pedagogie du Français langue étrangère
5.2.2 Les Méthodes dôenseigner le Français langue étrangère
5.2.3 Des documents pour lôenseignement
5.2.4 Préparation pour lôenseignement
5.2.5 Matériels didactiques
5.2.6 Evaluation

# 624 COMMUNICATION SKILLS

## 1.0 INTRODUCTION

This Communication Skills Examination Format is the result of the introduction of Communication Skillls subject which targets teacher education trainees who are expected to teach in primary school. The examination is intended to assess the candidateŝ ability to communicate using English Language.

## 2.0 GENERAL COMPETENCE

The Communication Skills examination will generally measure the candidatesô ability to:

2.1 apply theories and principles of Communication Skills.
2.2 develop and apply skills of oral presentations, discussions, writing composition, CV, minutes, and reports.
2.3 read and write notes from different sources.
2.4 search and interpret information from various sources.

## 3.0 SPECIFIC COMPETENCES

The examination will test the candidatesô ability to:

3.1 apply the four language skills: Listening, Speaking, Reading and Writing.
3.2 use Communication Skills effectively in various situations/settings.
3.3 make effective oral presentations.
3.4 write good compositions, CV, minutes, memos and reports.
3.5 apply participatory approaches in the teaching and learning of Communication Skills.

## 4.0 EXAMINATION RUBRIC

Communication Skills Examination will consist of **eighteen** (**18**) questions in sections A and B. The candidates will be required to answer **fourteen** (**14**) questions. The duration of the paper will be **three** (**3**) hours.

4.1 **Section A** will consist of **ten (10)** short answer questions with a total of **forty (40)** marks. The candidates will be required to answer **all** the questions.

4.2 **Section B** will consist of **eight** (**8**) essay type questions. Candidates will be required to answer **four** (**4**) questions. The section will carry **sixty** (**60**) marks.

## 5.0 EXAMINATION CONTENT

In setting the examination, the following topics will be considered:

5.1 Communication theory
5.2 Searching for information
5.3 Taking and making notes
5.4 Oral presentation
5.5 Reading skills
5.6 Writing skills
5.7 Tests and examinations

## 632 SAYANSI

### 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii inachukua nafasi ya fomati ya Sayansi iliyokuweko hapo awali ambayo iliweka mkazo katika kupima uwezo wa wahitimu wa Mafunzo ya Ualimu katika matumizi ya mbinu na njia anuwai za kufundishia somo la Sayansi. Fomati hii inatokana na maboresho ya mtaala wa Sayansi yaliyofanyika mwaka 2009 ambapo mada za taaluma ya somo la Sayansi zimeingizwa katika mtaala huo.

### 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa somo la Sayansi utapima ujuzi wa mtahiniwa katika:

2.1 uwezo wa kutumia stadi na mbinu shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sayansi.
2.2 kubuni mbinu bora za ufundishaji na ujifunzaji zinazozingatia usawa wa kijinsia, kinadharia na vitendo katika somo la Sayansi.
2.3 kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuwa na mwelekeo chanya kuhusu somo la Sayansi.
2.4 kutumia stadi na maarifa katika kubaini masuala mtambuko.
2.5 kuelewa stadi na matumizi ya Hisabati na mawasiliano katika somo la Sayansi.
2.6 kujiendeleza kitaaluma katika somo la sayansi.

### 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani wa somo la Sayansi utapima ujuzi wa mtahiniwa katika:

3.1 kuandaa masomo kwa kutumia mbinu shirikishi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa Sayansi.
3.2 kutengeneza na kufaragua zana na vifaa mbalimbali vya kujifunzia.
3.3 kuwaongoza wanafunzi katika kukusanya na kutengeneza zana na vifaa vya kujifunzia.
3.4 kumudu maudhui/mada za kitaaluma zilizoainishwa katika muhtasari wa somo la Ualimu Ngazi ya Cheti.
3.5 kuchambua na kutumia zana na vifaa katika ufundishaji.
3.6 kubainisha mbinu za kutathmini maendeleo ya mwanafunzi katika kufundisha na kujifunza somo la Sayansi.

### 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa Sayansi utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na nane** (**18**). Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne** (**14**). Muda wa mtihani huu ni saa **tatu** (**3**).

4.1 **Sehemu A** itakuwa na maswali **kumi** (**10**) yenye maswali ya majibu mafupi katika somo la Sayansi. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote** na jumla ya alama zitakuwa **arobaini** (**40**).

4.2 **Sehemu B** itakuwa na maswali **manne** (**4**) ya insha ambayo yatatahini mada za taaluma ya somo la Sayansi. Mtahiniwa atajibu maswali **mawili** (**2**). Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **thelathini** (**30**).

4.3 **Sehemu C** itakuwa na maswali **manne** (**4**) ya insha ambayo yatatahini mada za mbinu za kufundishia somo la Sayansi. Mtahiniwa atajibu maswali **mawili** (**2**). Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **thelathini** (**30**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani mada zifuatazo zitazingatiwa:

5.1 Afya na njia za kujikinga na magonjwa
5.2 Huduma ya kwanza
5.3 Viumbe hai
5.4 Nishati
5.5 Maada
5.6 Mashine rahisi
5.7 Mifumo ya mwili
5.8 Ufundishaji na ujifunzaji katika somo la Sayansi
5.9 Usimamizi wa maabara
5.10 Maandalizi ya ufundishaji
5.11 Ufundishaji
5.12 Upimaji

## 634 STADI ZA KAZI

### 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya mtihani wa somo la Stadi za Kazi imeandaliwa ili kwenda sanjari na mada zilizomo katika muhtasari mpya wa somo la Stadi za Kazi ngazi ya Cheti wa mwaka 2009. Mtihani wa Stadi za Kazi unaweka mkazo katika kupima ujuzi, stadi na mbinu zinazotakiwa ili kumudu mada mbalimbali zinazofundishwa katika somo hili kwa ngazi ya shule za msingi.

### 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa Stadi za Kazi unalenga kupima ujuzi wa watahiniwa katika:

2.1 kuelezea dhana, nadharia, kanuni na stadi mbalimbali alizojifunza katika somo la Stadi za Kazi.
2.2 kutambua maarifa na stadi za utafiti katika kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi.
2.3 kuelezea maarifa na stadi zinazohitajika katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi.
2.4 kukuza maarifa na stadi zinazohusu dhana mbalimbali za Stadi za Kazi.

### 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani wa Stadi za Kazi unalenga kupima ujuzi wa watahiniwa katika:

3.1 kufafanua nyanja mbalimbali za somo la Stadi za Kazi
3.2 kutumia maarifa yatokanayo na Stadi za Kazi kukuza uchumi wao
3.3 kutumia misingi ya somo la Stadi za Kazi kufundisha somo kikamilifu
3.4 kuzingatia umuhimu wa kufundisha somo la Stadi za Kazi
3.5 kufundisha kwa ufanisi mada zote za Stadi za Kazi
3.6 kuchopeka masuala mtambuko katika mada mbalimbali za Stadi za Kazi

### 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa Stadi za Kazi utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na nane (18)**. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne (14)** kwa muda wa saa **tatu (3)**.

4.1 **Sehemu A** itakuwa na maswali **kumi (10)** ya majibu mafupi na itakuwa na jumla ya alama **arobaini (40).** Maswali hayo yatahusu taaluma na mbinu za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**.

4.2 **Sehemu B** itakuwa na maswali **manne** (**4**) ya insha yatakayohusu taaluma ya somo la Stadi za Kazi. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **mawili (2).** Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **thelathini** (**30**).

4.3 **Sehemu C** itakuwa na maswali **manne** (**4**) ya insha yatakayohusu Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia somo la Stadi za Kazi. Mtahiniwa atajibu maswali **mawili** (**2**). Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **thelathini** (**30**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani mada zifuatazo zitazingatiwa:

5.1 Usanii wa picha, chapa, maumbo na mapambo
5.2 Ususi
5.3 Sanaa za maonesho
5.4 Ushoni wa nguo
5.5 Muziki
5.6 Kilimo, ufugaji na uvuvi
5.7 Upishi
5.8 Udobi
5.9 Upigaji picha
5.10 Biashara ndogo ndogo
5.11 Ufundi
5.12 Misingi ya kufundisha somo la stadi za kazi
5.13 Maandalizi ya ufundishaji
5.14 Ufundishaji
5.15 Upimaji

## 636 TEHAMA

### 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya mtihani wa somo la TEHAMA imeandaliwa ili kwenda sanjari na mada zilizomo katika muhtasari wa somo la TEHAMA ngazi ya Cheti wa mwaka 2009. Mtihani wa somo la TEHAMA unaweka mkazo katika kupima ujuzi, stadi na mbinu zinazotakiwa ili kumudu mada mbalimbali zinazofundishwa katika somo hili kwa ngazi ya shule za msingi.

### 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa somo la TEHAMA unalenga kupima uwezo wa watahiniwa katika:

2.1 kujenga stadi za kubuni, kutengeneza na kutumia vielelezo vya kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA katika shule za Msingi.
2.2 kutambua mbinu za uchambuzi wa vifaa vya mtaala wa somo la TEHAMA kwa shule za Msingi.
2.3 kuandaa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.
2.4 kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.
2.5 kutumia TEHAMA kukuza ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha.
2.6 kupima maudhui kwa kutumia jedwali la utahini.
2.7 kutumia TEHAMA kukuza maarifa na stadi katika kushughulikia masuala mtambuko.

### 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani wa somo la TEHAMA unalenga kupima ujuzi wa watahiniwa katika:

3.1 kutumia teknolojia na vielelezo katika ufundishaji na ujifunzaji.
3.2 kuainisha mada za muhtasari wa TEHAMA na vitabu vya kiada na ziada kwa shule za msingi.
3.3 kuandaa na kutumia azimio la kazi na andalio la somo katika ufundishaji na ujifunzaji somo la TEHAMA.
3.4 kutumia misingi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.
3.5 kuandaa mazoezi, majaribio na mitihani yenye kukidhi majazi yote ya kielimu.

### 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa somo la TEHAMA utakuwa na sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nane** (**18**). Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne (14)** kwa muda wa saa **tatu** (**3**).

4.1 **Sehemu A** itakuwa na maswali **kumi** (**10**) ya majibu mafupi kutoka katika mada zote za somo la TEHAMA ambapo mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **arobaini (40)**.

4.2 **Sehemu B** itakuwa na maswali **nane** (**8**) ya insha na mtahiniwaatatakiwa kujibu maswali **manne (4).** Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **sitini** (**60**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani, mada kuu zifuatazo zitazingatiwa:

5.1 misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la TEHAMA
5.2 maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA
5.3 ufundishaji wa masomo ya mfano
5.4 upimaji

## 638 VIELELEZO NA TEKNOLOJIA

### 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya mtihani wa somo la Vielelezo na Teknolojia imeandaliwa ili kwenda sanjari na mada zilizomo katika muhtasari mpya wa Vielelezo na Teknolojia ngazi ya Cheti wa mwaka 2009. Mtihani wa Vielelezo na Teknolojia unaweka mkazo katika kupima ujuzi, stadi na mbinu zilizolengwa ili kumudu mada mbalimbali zinazofundishwa katika somo hili kwa ngazi ya shule za msingi.

### 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa somo la Vielelezo na Teknolojia unalenga kupima uwezo wa watahiniwa katika:

2.1 kukuza ubunifu wa kuandaa Vielelezo na Teknolojia maono, masikizi na masikizi-maono.
2.2 Kubainisha aina mbalimbali za Vielelezo na Teknolojia wanavyoweza kufaragua, kutengeneza na kutumia kwa kufundishia na kujifunzia.
2.3 kubainisha sifa za kuzingatia katika utengenezaji wa Vielelezo na Teknolojia bora na fanisi.
2.4 kubainisha aina za Vielelezo na Teknolojia bora na fanisi.
2.5 kueleza njia mbalimbali za utunzaji na usalama wa Vielelezo na Teknolojia.
2.6 kutumia aina mbalimbali za utunzaji na usalama wa Vielelezo na Teknolojia.

### 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani unalenga kupima ujuzi wa watahiniwa katika:

3.1 kutambua mbinu mbalimbali na kuzitumia katika kufaragua na kutengeneza Vielelezo na Teknolojia ya kufundishia na kujifunzia.
3.2 kuhifadhi Vielelezo na Teknolojia mbalimbali za kufundishia na kujifunzia.
3.3 kubuni aina mbalimbali za Vielelezo na Teknolojia kwa kutumia malighafi inayopatikana katika mazingira anamoishi.
3.4 kutambua aina mbalimbali za Vielelezo na Teknolojia zinazoweza kutengenezwa na kutumika katika kufundishia na kujifunzia.

### 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa Vielelezo na Teknolojia utakuwa na sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nane (18).** Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne (14).** Muda wa mtihani huu ni saa **tatu** (**3**).

4.1 **Sehemu A** itakuwa na maswali **kumi** (**10**) ya majibu mafupi kutoka katika mada zote za Vielelezo na Teknolojia ambapo mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote**. Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **arobaini** (**40**).

4.2 **Sehemu B** itakuwa na maswali **nane** (**8**) ya insha kutoka katika mada za somo la Vielelezo na Teknolojia. Mtahiniwa atajibu maswali **manne (4)** yenye jumla ya alama **sitini** (**60**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani, mada kuu zifuatazo zitazingatiwa:

5.1 Misingi ya kubuni, kufaragua na kutengeneza Vielelezo na Teknolojia

5.2 Vielelezo na Teknolojia kwa kufundishia na kujifunzia

5.3 Aina za Vielelezo na Teknolojia

5.4 Makundi ya Vielelezo na Teknolojia

5.5 Mbinu za kufaragua na kutengeneza Vielelezo na Teknolojia kwa kufundishia na kujifunzia

5.6 Matumizi ya Vielelezo na Teknolojia katika kufundishia na kujifunzia

## 640 HISABATI

### 1.0 UTANGULIZI

Marekebisho ya fomati hii ya somo la Hisabati yamefanyika kwa kuzingatia muhtasari uliorekebishwa wa mwaka 2009. Muhtasari uliorekebishwa umejumuisha mada za taaluma na mada za ufundishaji wa somo la Hisabati. Fomati hii inatilia mkazo kumpima mtahiniwa ujuzi, stadi na mbinu shirikishi katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa somo la Hisabati.

### 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa somo la Hisabati unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 kukuza uelewa wa kanuni na nadharia za Hisabati.
2.2 kutafsiri maana ya dhana za Hisabati, kukokotoa Hisabati na kueleza uhusiano wake katika nyanja nyingine za maisha zikiwemo stadi za mawasiliano na Teknolojia.
2.3 kutumia maarifa na stadi za Hisabati katika kutatua matatizo katika maisha ya kila siku yakiwemo masuala mtambuka.
2.4 kuchambua muhtasari na vifaa vya muhtasari wa Hisabati.
2.5 kupima na kutathmini maendeleo ya ujifunzaji wa Hisabati na kutoa mrejesho.

### 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani utapima uwezo wa watahiniwa katika:

3.1 kueleza maana ya dhana za kihisabati zilizoorodheshwa katika Muhtasari.
3.2 kukokotoa Hisabati.
3.3 kueleza uhusiano wa mada mbalimbali za Hisabati.
3.4 kueleza na kukadiria thamani ya dhana zote za kihisabati kama zilivyoorodheshwa katika Muhtasari.
3.5 kubaini uhusiano kati ya mitajo, mionyesho, milinganyo sahili.
3.6 kufumbua mafumbo yanayohusu Hisabati.
3.7 kutumia njia mbalimbali za kufundishia na kujifunzia.
3.8 kuchambua vifaa vyote vya Mtaala wa Hisabati.
3.9 kuandaa somo la Hisabati.
3.10 kutathmini somo la Hisabati.

### 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Mtihani wa Hisabati utakuwa na sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na nane** (**18**). Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne** (**14**). Muda wa mtihani huu ni saa **tatu** (**3**).

4.1 **Sehemu A** itakuwa na maswali **kumi** (**10**) ya majibu mafupi yatakayotokana na mada zote za somo la Hisabati. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **yote.** Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **arobaini** (**40**).

4.2 **Sehemu B** itakuwa na maswali **matano** (**5**) yatakayotahini maudhui ya taaluma ya Hisabati.

4.3 **Sehemu C** itakuwa na maswali **matatu** (**3**) yatakayotahini maudhui ya Mbinu za Kufundishia Hisabati. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **mawili** (**2**). Sehemu hii itakuwa na jumla ya alama **thelathini** (**30**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani mada zifuatazo zitazingatiwa:

5.1 Namba nzima
5.2 Sehemu
5.3 Vipimo
5.4 Jometri
5.5 Namba kamili
5.6 Aljebra
5.7 Takwimu
5.8 Kukadiria
5.9 Hesabu za biashara
5.10 Seti
5.11 Misingi ya ufundishaji na ujifunzaji somo la Hisabati
5.12 Maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji somo la Hisabati
5.13 Ufundishaji wa mada teule
5.14 Upimaji katika Hisabati

## 650 HAIBA NA MICHEZO

### 1.0 UTANGULIZI

Fomati hii ya mtihani wa somo la Haiba na Michezo inatokana na muhtasari mpya wa somo la Haiba na Michezo ambao umeanza kutumika kwa mara ya kwanza katika vyuo vya ualimu mwaka 2009. Somo la Haiba na Michezo linalenga kujenga uwezo wa wanachuo katika stadi za uchezaji wa michezo mbalimbali na ujenzi wa stadi hizo kwa wanafunzi. Aidha, mtihani unakusudia kuwapima watahiniwa uwezo wao wa kujijengea stadi na maarifa ya kushughulikia masuala mtambuka na wanafunzi wenye mahitaji maalum kwenye somo la Haiba na Michezo.

### 2.0 UJUZI WA JUMLA

Mtihani wa Haiba na Michezo unalenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika:

2.1 kutumia mbinu za michezo kwa ufanisi katika ufundishaji utakaowawezesha wanafunzi kujifunza.
2.2 kutumia mbinu sahihi za michezo katika ufundishaji na ujifunzaji.
2.3 kutumia maarifa, stadi na mielekeo katika kushughulikia masuala mtambuka.
2.4 kupima na kutathmini ufundishaji na ujifunzaji wa somo.
2.5 kuandaa, kuchambua na kutumia vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia kwa ufanisi.
2.6 kutumia mazingira katika ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.
2.7 kuendesha tafiti ndogo za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.

### 3.0 UJUZI MAHUSUSI

Mtihani wa Haiba na Michezo unalenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika:

3.1 kubuni, kufaragua, kutengeneza, kutumia zana/vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.
3.2 kushirikisha wanafunzi wenye mahitaji mbalimbali katika mchakato wa kufundisha na kujifunza.
3.3 kutambua na kutatua matatizo mbalimbali ya wanafunzi katika kufundisha.
3.4 kuchopeka masuala mtambuka wakati wa kufundisha mada mbalimbali za somo la Haiba na Michezo.
3.5 kutumia tafiti ndogo kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.
3.6 kupima na kutathmini maarifa, ujuzi na mchakato wa kufundisha somo la Haiba na Michezo.

### 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

4.1 Mtihani wa Haiba na Michezo utakuwa na sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nane** (**18**). Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali **kumi na nne** (**14**) kwa muda wa saa **tatu** (**3**).

4.2 **Sehemu A** itakuwa na maswali **kumi** (**10**) yanayotoka katika mada ya somo la Haiba na Michezo yenye jumla ya alama **arobaini** (**40**). Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali yote kwa kutoa majibu mafupi.

4.3 **Sehemu B** itakuwa na maswali **nane** (**8**) ya insha yatakayotokana na mada za somo la Haiba na Michezo. Mtahiniwa atajibu maswali **manne (4)** yenye jumla ya alama **sitini** (**60**).

## 5.0 MAUDHUI YA MTIHANI

Katika kuandaa mtihani mada zifuatazo zitazingatiwa:

5.1 Misingi ya ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.
5.2 Maandalizi ya maandiko, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia.
5.3 Zana za kufundishia na kujifunzia.
5.4 Maandalizi ya ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.
5.5 Upimaji na tathmini ya ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.